

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**



**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**MKOA WA SINGIDA**

**TAARIFA FUPI KUHUSU MKOA WA SINGIDA**

*Imetayarishwa na:-*  
Ofisi ya Mkuu wa Mkoa,  
S.L.P. 05,  
SINGIDA.

Simu Na. 026-2502170/2249  
Nukushi Na. 026-2502078/2991  
Barua pepe: [ras@singida.go.tz](mailto:ras@singida.go.tz)

Julai, 2017

## **TAARIFA KUHUSU MKOA WA SINGIDA**

---

- 1 Mkoa wa Singida una ukubwa wa eneo ni Km **49,438** za mraba , ikiwa km **49,342.50** ni eneo la Nchi kavu na km **95.50** ni eneo la maji.
- 2 Mkoa una Idadi ya watu (Makadirio ya Idadi ya Watu kwa takwimu za mwaka 2017 wapatao watu **1,551,767**.
- 3 Kiwango cha ongezeko la watu kwa kila mwaka ni wastani wa asilimia 2.3
- 4 Pato la Mkoa wa Singida mwaka 2016, kwa mujibu wa takwimu kutoka Ofisi ya Taifa ya takwimu (NBS) ni Shs Trilioni **1.919**, wakati Pato la kila mwananchi ni Shs **1,275,102** kwa mwaka.
- 5 Mkoa wa Singida umechangia wastani wa asilimia **1.85** kwenye Pato la Taifa kwa mwaka 2016.
- 6 Uzalishaji wa mazao ya chakula kufikia Juni mwaka 2016/2017 ni tani **457,104.7**, na uvunaji unaendelea kwa baadhi ya maeneo.
- 7 Uzalishaji wa alizeti kufikia Juni mwaka 2016/2017 ni tani 167,725, hii ni sawa na asilimia **68.3** ya matarajio ya mavuno ambayo ilikuwa ni kuvuna tani **245,458**. Uzalishaji haukufikia malengo kutokana na upungufu wa mvua.
- 8 Mkoa wa Singida kwa kufikia mwezi Juni mwaka 2017 unakadiriwa kuwa na jumla ya ng'ombe wapatao **1,037,794**.
- 9 Mkoa wa Singida una viwanda vya usindikaji wa Mafuta ya alizeti 120; vikubwa **2**, kati ya hivyo kiwanda 1 kipo katika hatua za mwisho za ujenzi, vya kati 3, vidogo **115**. Viwanda vyote vya kusindika alizeti vina uwezo wa kusindika Tani 434,725. Hali halisi ya upatikanaji wa malighafi ya alizeti ndani ya Mkoa ni wastani wa Tani 160,000, sawa na asilimia 37 ya mahitaji ya malighafi hadi kufikia mwezi Juni, 2017. Hivyo kuna upungufu wa malighafi wa tani 274,725.
- 10 Mkoa una Vituo 21 vya mafuta, baadhi vina mashine ya ki-eletronic ya kutolea risiti. Aidha, vituo vilivyosalia tayari vimeshalipia mashine hizo ingawa Muuzaji (Supplier) hajawapatia.
- 11 Mkoa unayo misitu ya hifadhi 3 inayohifadhiwa chini ya Vijiji, yenye eneo la Hekta 339,369. Misitu hiyo ni Minyughe (Ha 270,000) uliyopo katika Halmashauri ya Ikungi, Mgori (Ha 39,000) uliopo katika Halmashauri ya Singida, Sekenke – Tulya (Ha 30,369) uliopo katika Halmashauri ya Iramba. Pia Mkoa una pori la akiba la Rungwa, Kizigo na Muhesi Wilayani Manyoni lenye jumla ya kilomita za mraba 15,836.

## **TAARIFA KUHUSU MKOA WA SINGIDA**

---

- 12 Idadi ya ng'ombe walio kwenye hifadhi za misitu na mapori ya akiba ni jumla ya ng'ombe 51,139, katika hifadhi ya msitu wa Minyughe kuna ng'ombe 10,300, hifadhi ya msitu wa Mgori kuna ng'ombe 12,000, na pori la akiba la Rungwa, Kizigo na Muhesi kuna ng'ombe 28,839.
- 13 Mkoa umejaliwa kuwa na madini katika meneo mbalimbali yapatayo 46. Madini yanayopatikana ni dhahabu, shaba, chuma, Titunium; urani, zircon, quartz, amethyst, garnet, kimberlite, almasi, madini ya chumvi, kifusi, mawe, gypsum, kokoto na mchanga. Kwa kiasi kikubwa uchimbaji unafanywa na wachimbaji wadogo.
- 14 Uzalishaji na thamani ya madini kwa mwaka 2016/2017; madini ya ujenzi uzalishaji wake ulikuwa tani 34,102.50 zenye thamani ya Shs 125,500,000, madini ya jasi uzalishaji wake ulikuwa tani 5,290.83 sawa na Shs 411,341,666.67, na dhahabu uzalishaji wake ulikuwa ni gram 31,383.26 sawa na Shs 2,089,659,445.5 na hivyo kufanya jumla ya mapato ya Shs 2,626,501,112.17.
- 15 Jumla ya mrabaha uliotolewa kwa mwaka 2016/2017 ni Shs 115,052,531, kwa madini ya dhahabu ni Shs 83,592,531.29, madini ya jasi ni Shs 12,437,000 na madini ya ujenzi ni Shs 19,023,000.